

# Wafugaji waomba ulinzi eneo la malisho

Mussa Juma, Mwananchi  
mjuma@mwananchi.co.tz

**Longido.** Mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini zimeanza kurejesha malisho ya mifugo, huku wafugaji wa Wilaya ya Longido wakitaka ulinzi wa kisheria wa eneo la hekta 186,794.2.

Katika kukabiliana na ukosefu wa malisho, Halmashauri ya Longido imeanza kugawa kilo 400 za mbegu za majani kwa mashamba

yaliyotengwa kuzalisha majani hayo.

Wakizungumza na *Mwananchi* jana, baadhi ya wafugaji na viongozi wa vijiji walisema mvua zili zoanza kunyesha zitasaidia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kutovamiwa.

Loshiye Kilau alisema wafugaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Longido wametenga maeneo ya malisho, hali itakayosaidia kuwa na majani ya kutosha.

"Mifugo zaidi ya 38,000 imekufa


mwaka jana wilayani kwetu, hatutaki kurudi tulikotoka, bali sasa tutumie maarifa yetu ya asili kuannda maeneo ya malisho ya muda mrefu lakini tunaomba tulindwe kisheria," alisema Kilau.

**"Wasiwe na hofu kuwa yatavamiwa, haya ni maeneo yao na watayasimamia wenye wekuhakikisha mifugo inapata malisho wakati wote na kuondoa adha ya mifugo kufa."**

Daqarro

Akizungumzia hilo, Ofisa Mifugo na Uvuvi Longido, Nestory Daqarro alisema kutengwa kwa maeneo ya malisho kutasaidia wafugaji kupata malisho ya uhakika.

Alisema programu hiyo inatekelezwa kuititia mradi wa uhifadhi wa mazingira kwa maarifa asilia unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuititia programu ya miradi midogo.



HABARI